Nyuma Ya Pazia inazungumzia ubadhirifu unaomhusisha rais na mawaziri wake katika nchi ya Mafuriko au Abracadabra. Rais akishirikiana na waziri mkuu walileta kampuni ya kigeni ya kuuwa wadudu ya Richmen kuwekeza kwenye kuzalisha umeme nchini Mafurikoni; Richmen to invest in power generation in Mafuriko. Kupitia rushwa na ushawishi wa wakubwa hawa Richmen ilipata tenda na kutumika kama mrija wa kuibia mabilioni ya fedha za umma toka Benki Kuu. Wananchi walipogundua jinai hii waliangusha serikali na kuwaaadhibu watawala wao kwa kuwafunga maisha na wengine kuhukumiwa vifo. Kitabu kinaupiga kijembe tawala fisadi barani Afrika.


254 pages | 203 × 127 mm | 2015

Publisher: Langaa RPCIG, Cameroon

Paperback: 9789956792184 \$22/£15/€19

Vutu ni kuvute

Shafi Adam Shafi



Shafi Adam Shafi aliyeandika Kasri ya Mwinyi Fuad na Kuli anainua kiwango na hadhi ya fasihi ya Kiswahili katika riwaya hii Vuta N' kuvute. Kwanza, kuna ndoa ya Yasmin, mtoto wa kihindi kwa Bwana Raza, mzee sawa na babu yake. Yasmin anafukuzwa na wazee wake kwa kumwacha Raza. Katika upweke wake anasitiriwa na Mwajuma, shoga yake anayeishi ili kustarehe katika dansa, taarab na pegi za vikali. Yasmin anaingizwa uswahilini. Kuna wivu unaopelekea kifo cha Shibab, mume wa pili wa Yasmin. Kuna Denge, Yasmin anampenda lakini hapendeki. Kwa Denge ni mapambano na ukoloni tu na makachero wake. Hii ni Vutu N' kuvute ambayo sherti yeye na wenzake waishinde.


277 pages | 203 × 130 mm | 1999

Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania

Paperback: 9789976973297 \$22/£16/€19

Vitimbi vya Mama wa Kambo: *na hadithi nyingine*

Ally Yusufu Mugenzi



Vitimbi vya Mama wa Kambo, Wivu, Radhi za Wazazi, Ra ki Maluuni, Mchumba Kaka na Adui Mama ni hadithi zinazosawiri jamii alimochipukia mwandishi, au kuishi na kufanya kazi akiwa polisi, mwandishi wa habari na mtangazaji wa redio katika nchi za Tanzania, Rwanda, Burundi na Uingereza kwa takriban miaka 40. Kitabu hiki ni matokeo ya maombi ya watu wengi waliomsikiliza akizisimulia katika kipindi cha Hadithi na Muziki cha Redio Rwanda katika miaka ya 1980 na 1990. Hadithi hizi pia zimekuwa zikitumiwa na wakuza mitaala wa Kiswahili nchini Rwanda shuleni na zimewafurahisha wapenzi wengine wa fasihi nje ya shule.

Ally Yusufu Mugenzi kwa jina jingine Ally Kayamba alijiunga na Chuo cha Uandishi wa Habari Tanzania mwaka 1978. Alipohitimu mwaka 1980, aliajiriwa na Shirika la Habari Tanzania - SHIHATA. Mwaka 1983 aliacha kazi SHIHATA akajiunga na Idhaa ya Kiswahili ya Redio Rwanda. Mwanzoni mwa mwaka 1994, aliacha kazi Radio Rwanda alipoajiriwa na Idhaa ya Kiswahili ya BBC-London. Akiwa BBC, alianzisha idhaa ya kukutanisha watu waliotenganishwa na mauaji ya kimbari ya Rwanda. Baadaye ilibadilika na kuwa Idhaa ya Maziwa Makuu. Mwaka 2005 aliteuliwa kuwa mhariri wa idhaa hiyo ambako yuko mpaka sasa.


162 pages | 198 × 129 mm | 2020

Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania

Paperback: 9789987084081 \$24/£18/€21

Diwani ya Tuzo ya Ushairi ya Ebrahim Hussein

Juzuu la Pili



Diwani hii ni matunda ya shindano la pili la Tuzo ya Ushairi ya Ebrahim Hussein lililofanyika mwaka 2015/16. Tuzo hiyo ilianzishwa na hayati Gerald Belkin, muongozo filamu aliyekuja Tanzania kutengeneza filamu juu ya maisha na changamoto za ujenzi wa ujamaa vijijini miaka ya 1960 na 1970.

Belkin alifanya kazi bega kwa bega na Profesa Ebrahim Hussein, mwanazuoni maarufu na mwandishi wa tamthilia na mashairi. Kupitia kwa Hussein, Belkin alivutiwa na utamaduni wa Kiswahili, hususani ushairi. Katika wosia wake, kabla ya kufikwa na mauti, aliacha fungu la fedha ili zitumiwe kushindanisha washairi wa Tanzania, na tuzo itolewe kwa washindi watatu wa kwanza. Belkin alianzisha tuzo hii ili kuenzi mchango wa rafiki yake, Ebrahim Hussein, katika kuijenga fasihi ya Kiswahili.

Ebrahim Hussein ametoa mchango mkubwa katika utunzi, uchambuzi na falsafa ya fasihi. Vitabu vyake, kwa mfano, Kinjeketile, Mashetani, Wakati Ukuta na Kwenye Ukingo wa Thim vimebeba fikra nzito juu ya migogoro ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni inayotokana na mabadiliko ya kihistoria nchini Tanzania na barani Afrika kabla na baada ya uhuru.

Mashairi haya yametungwa na washairi mchanganyiko – vijana, watu wazima, wazee, wanawake, wanaume, wafanyakazi, wasomi, wakulima, n.k. Kwa pamoja, mashairi haya yanatusawiria hali ya Tanzania na Afrika katika kipindi hiki, na kubainisha mitazamo anuai ya wananchi wa kawaida kuhusu hali hiyo na kuhusu mustakabali wa nchi yao na bara lao la Afrika. Diwani hii inafaa kusomwa na watu wote wanaojali hali na hatima ya Mwafrika.


105 pages | 203 × 133 mm | 2010 | vielelelezovya rangi

Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania

Paperback: 9789987083268 \$24/£18/€21

Kale ya Washairi wa Pemba: *Kamange na Sarahani*

Mhariri: Abdilatif Abdala



Abdilatif Abdalla mhariri wa kitabu hiki ni mwandishi wa Kenya na mwanaharakati wa kisiasa. Alifungwa gereza kwa kuunga mkono Umoja wa Wananchi wa Kenya, na akiwa kifungoni aliandika mashairi yaliyokusanywa katika kitabu, Sauti ya Dhiki, ambayo baadaye yalipewa Tuzo ya Jomo Kenyatta ya Fasihi. Baada ya kuachiliwa kutoka gereza mnamo 1972 aliondoka Kenya na kufanya kazi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania na baada ya hapo akafanya kazi kwenye idhaa ya Kiswahili ya BBC, London. Baadaye aliteuliwa kuwa Mwalimu wa Kiswahili katika Idala ya Mafunzo ya Mashariki na Afrika katika Chuo Kikuu cha London na, hivi karibuni, katika Chuo Kikuu cha Leipzig Ujerumani. Alistaafu mwaka 2011. Mwaka 2018 alipewa Tuzo ya Fonlon-Nichols ya Chama cha Fasihi ya Afrika.

Kale ya Washairi wa Pemba ni mkusanyiko mkubwa wa utajiri wa mashairi yenye kuchanganya lahaja mbalimbali za Kipemba, Kimvita, Kiamu, Kimrima, Kivumba na yametumia pia maneno yenye asili ya Kiarabu yatumikayo katika Kiswahili.

Kale ya Pemba ni kale ya Waswahili na mazingira yao. Maandiko machache ya Abdulrahman Saggaf Alawy na Ali Abdalla El Maawy yameonesha mazingira ya watu wa kale na mawazo yao. Kale hiyo si kale ya kabla ya Fumo Liyongo, bali ni kale ya akina Kamange na Sarahani. Kamange na Sarahani waliingia katika karne ya kumi na tisa na kufariki katika karne ya ishirini. Mashairi yao yalivuma pwani yote ya Afrika Mashariki. Mwandishi Abdulrahman Saggaf Alawy amefanikiwa kukusanya baadhi tu ya maandiko ambayo yote yameandikwa katika mtindo wa kale wenye kujali bahari ya vina, mizani na kibwagizo cha wazo moja. Kamange alipenda sana kutunga mashairi ya kujitoma, ya ushaha, ya utendaji na ukali wa mapenzi ya wanawake. Sarahani alipenda elimu na kusomesha, kuingia katika falsafa na kutoa mawaidha.


Mashairi ya washairi hawa ni changamoto kubwa kwa wasomi wa Kiswahili wa ushairi kwa upeo wa juu sana wa sanaa na umahiri wa lugha.

150 pages | 229 × 152 mm | 2012

Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania

Paperback: 9789987082827 \$24/£18/€21

eBook: 9789987081608 \$11/£8/€10




Diwani ya Jinamizi

Ali Salim Zakwany

Kitabu hiki kina tungo za mshairi Ali Salim Zakwany. Tungo zake zimesheheni maarifa na hekima maridhawa kwani zagusa nyanja zote ya maisha ya watu: Maadili, Elimu, Siasa, Dini n.k.

128 pages | 204 × 145 mm | 2004

Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania | Paperback: 9789987686780 \$24/£18/€21




Diwani ya Mloka

Charles Mloka

Diwani ya Mloka ni mkusanyiko wa mashairi yanayozungumzia masuala mbalimbali ya kijamii na yanayomwandaa msomaji katika misingi bora kimaisha; kuchochea hamasa na juhudi za kuendeleza Kiswahili; na kuhifadhi mashairi yanayoakisi migogoro mbalimbali ya kisiasa, kijamii na kiuchumi iliyokuwepo wakati wa utawala wa chama kimoja nchini Tanzania. "Hatua hii ya Mloka ni ya kufaa kuigwa...".

94 pages | 205 × 147 mm | 2002

Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania | Paperback: 9789987686445 \$24/£18/€21



Diwani ya Ustadhi Nyamaume

Khamis Amani Nyamaume


Mkusanyiko wa mashairi ya mmoja kati ya washairi maarufu na waliopendwa, Khamis Amani Nyamaume. Alifahamika kwa uwezo wake wa kutunga mashairi juu ya mada nyingi na tofauti na katika mapana ya aina za mashairi. Kwa sababu hiyo na nyingine Khamis Nyamaume alipendwa na wasomaji wa rika zote. Washairi wenzake walikuwa akina Shaaban Robert, Mathias Mnyampala, Sheikh Kaluta Amri Abedi, Hassan Mbega, Mdanzi Hanasa na Mahmood Hamdouny na wote hawa walithamini sana ushairi wake.

132 pages | 210 × 148 mm | 2004 | Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania

Paperback: 9789987686834 \$24/£18/€21

DOA

Kithaka wa Mberia



Profesa Kithaka wa Mberia anafundisha na kufanya utafiti katika Idara ya Isimu na Lugha, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya. Mbali na kufundisha na kufanya utafiti, anajishughulisha na uandishi wa mashairi na tamthilia. Tamthilia yake maarufu iitwayo Kifo Kisimani ilikuwa kitabu cha lazima katika mtihani wa kidato cha nne nchini Kenya kuanzia 2006 hadi 2012. Tamthilia yake nyingine iitwayo Natala ilikuwa kitabu cha kutahiniwa katika vyuo vya walimu, pia nchini Kenya, kuanzia 2005 hadi 2016. Mwandishi amewahi kukariri mashairi yake katika maeneo kadhaa ikiwa ni pamoja na Kenya, Tanzania, Iran, Marekani, US Virgin Islands, United Arab Emirates, Upolanzi, Ujerumani na Italia.


130 pages | 178 × 127 mm | 2018

Publisher: Marimba Publications, Kenya

Paperback: 9789966794420 \$16/£12/€13

Mvumo wa Helikopta

Kithaka wa Mberia



Prof. Kithaka wa Mberia anafundisha na kufanya utafiti katika Idara ya Isimu na Lugha, Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi, Kenya. Amewahi kufundisha Virginia State University, Marekani, kama Fulbright Scholar-in-Residence; University of Warsaw, Upolanzi; na hivi sasa anafundisha Hankuk University of Foreign Studies, Korea Kusini.

Mbali na Mvumo wa Helikopta, Kifo Kisimani na Natala, Prof. Kithaka wa Mberia amechapisha vitabu vingine ambavyo ni Mchezo wa Karata (mashairi), Bara Jingine (mashairi), Redio na Mwezi (mashairi), Msimu wa Tisa (mashairi), Rangi ya Anga (mashairi), Doa (shairi) na Maua Kwenye Jua la Asubuhi (tamthilia).


94 pages | 178 × 127 mm | 2019

Publisher: Marimba Publications, Kenya

Paperback: 9789789966400 \$16/£12/€13

Mtawa Mweusi

Ngugi wa Thiong'o



Yampasa Remi, wa kwanza wa kabila lake kupata masomo ya chuo kikuu, kurudi kwa watu wake? Yampasa kumrudia Thoni, mjane wa nduguye, ambaye ilimbidi kumwoa kufuatana na mila za kikabila? Au aendelee kuwa mtawa mweusi mjini, akitembelea vilabu vya usiku pamoja na rafiki yake Jeni? Yampasa kukitetea Chama cha Mwafrika hali watu wake wanaona kwamba mahali pa dhuluma za kikoloni, zimeanzishwa tu dhuluma za aina ingine mpya? Haya ndiyo mapingano ya maswali kwenye huu mchezo ambao umekwisha igizwa katika sehemu nyingi Afrika na ng'ambo.

94 pages | 203 × 127 mm | 2010


Publisher: East African Educational Publishers, Kenya

Paperback: 9789987083268 \$24/£18/€21

Watoto Wamama Mudu

Tamthiliya Tanzania Ramsa kutoka Afrika Kusinibaada ya Uhuru

Masitha Hoeane



Jumuiya ya Edladleni inajitahidi kujikubali katika Afrika Kusini baada ya uhuru wakati wanapoogelea dhidi ya wimbi la umuhimu wa kuishi na mamilioni ya matarajio yaliyokwamishwa. Safari za wahusika zinajumuisha mzozo na utelezi kutoka kwa kunyimwa, chuki dhidi ya wageni, uhalifu, kusambaratika kwa kitengo cha familia, kujitenga na ubinafsi na jamii, uzembe, na uchungu wa kujiharibu. Walakini hata katika kina cha ukombozi wa kukata tamaa bado kunawezekana katika mapumziko ya maadili ya Ubuntu-binadamu, roho ya jamii na harakati za mazingira.

104 pages | 210 × 148 mm | 2017


Publisher: African Perspectives, South Africa

Paperback: 9780639918730 \$57/£45

Tamthilia Mbili za Kifaransa

Victor Hugo, Jean-Luc Luc Lagarce

Mfasiri: Marcel Kalunga Mwela



Professor Marcel Kalunga Mwela-Ubi ni raia wa Jamuhuri ya Kidemokrasi ya Congo na tafsiri hizi zilishinda na kupewa tuzo katika mashindano ya kutafsiri tamthilia za Kifaransa katika Kiswahili. Kwa jinsi maandiko yenyewe yalivyo na mvuto mkubwa, baada ya kusoma kurasa chache na kuzoea matumizi ya Kiswahili cha Congo (Kingwana), msomaji atazama katika uhondo wa ucheshi wa tamthilia hizi na kugundua kuwa, kumbe si lazima, waandishi wote watumie Kiswahili sanifu.

Victor Hugo (1802–1855) alikubalika kuwa mshairi bora wa Ufaransa na mwandishi wa pekee kabisa wa tamthilia, riwaya na insha. Anahesabika kuwa mmoja wa waandishi maarufu kabisa kutoka Ufaransa.

Jean-Luc Lagarce (1957–1995) “Kanuni kwa kuishi maisha ya kisasa” ni mmoja wa michezo yake ya kuigiza ambayo imemfanya kuwa msanii anayeongoza katika michezo inayoonyeshwa kwenye majukwaa nchini Ufaransa katika miongo ya mwisho ya karne ya ishirini.


150 pages | 198 × 129 mm | 2013

Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania

Paperback: 9789987083268 \$24/£18/€21

Mkwamo

Masereka Levi Kahaika



Mkwamo ni tamthilia ya Kiswahili iliyoandikwa na Masereka Levi Kahaika na iliyochapishwa mwaka 2013. Kwa kiasi kikubwa Mkwamo wa kupendeza umejengwa kwa sehemu juu ya msingi wa falme mbili zilizopo za Kasulenge na Bupomboli, ambazo zinawakilisha falme za Buganda na Bunyoro wakati wa ukoloni nchini Uganda. Mchezo huo pia unaangazia mauaji ya Mashahidi wa Uganda; jinsi na kwa nini yalitokea. Mchezo huo huwapa wasomaji mtazamo wa kuchanganyikiwa kati ya wafalme wa wakati huo na wakoloni, na kutafakari juu ya mbegu za udini katika ya jamii ya Waganda.


94 pages | 210 × 148 mm | 2018

Publisher: Fountain Publishers, Uganda

Paperback: 9789970252954 \$20/£15/€18

Kamusi ya Ukristo

Jordan Nyenyembe



Jordan Nyenyembe ni mwanatheolojia Mkatoliki na kuhani wa Dayosisi ya Mbinga nchini Tanzania. Amesoma katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino cha Tanzania na Chuo Kikuu cha Vienna mtawaliwa; ambapo alipata jina lake la Udaktari katika Kitivo cha Theolojia Katoliki. Hivi sasa, anafanya kazi ya kichungaji katika Parokia ya Mtakatifu Alois Gonzaga katika Dayosisi ya nyumbani kwake.

Kamusi yoyote ni kazi ya maarifa, ni chemchemi ambayo maji yake hayakauki, hutiririsha maarifa na kuchochea watumiaji kutaka kuijua zaidi.

Kamusi ya Ukristo inazo sifa hizi, na za ziada kwani ni kamusi ya kwanza kwa lugha ya Kiswahili ambayo inaweka pamoja, tafsiri ya dhana mbalimbali, majina mbalimbali ya Wakristo na desturi za Makanisa ya Kikristo.

Kamusi ya Ukristo ni kamusi ambamo kwa umahili mkubwa mwandishi amefuatilia na kufanikiwa kukusanya vitomeo vinavyowakilisha madhehebu mbalimbali ya Kikristo. Kuna vidahizo ambavyo hutumiwa zaidi na dhehebu moja kuliko lingine, lakini mwandishi ameviweka pamoja ili kuuondoa umadhehebu na kuujenga umoja wa Ukristo. Ni ukweli usiopingika kuwa waamini wengi hawaelewi misamiati na istilahi nyingi za dini zao. Hivyo basi kwa msaada wa Kamusi hii msomaji atafaidi maarifa ya maana na matumizi ya maneno si tu ya dhehebu moja, dhehebu lake, bali Ukristo kwa ujumla wake.


322 pages | 178 × 127 mm | 2016

Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania

Paperback: 9789987753178 \$34/£24/€28

Kamusi Angaza, Shule za Msingi


Ahmed E. Ndalu



Hii ni kamusi ya Kiswahili inayowalenga wanafunzi wa msingi wa lugha hiyo. Ni zao la utafiti mpana uliofanywa na mwandishi na kukaguliwa sana na waandishi wa kamusi wenye uzoefu kutoka Afrika Mashariki. Baadhi ya huduma muhimu zinazofanya kamusi hii kuwa bora ni pamoja na: zaidi ya vichwa vya maneno 7,000; Maneno 170,000, madarasa ya nomino yaliyofafanuliwa wazi, na faharisi ambayo inajumuisha vielelezo vya rangi ya aina tofauti za wanyama, maumbo, rangi, na ndege.

384 pages | 210 × 148 mm | 2011 | vielelelezovya rangi
 Publisher: East African Educational Publishers, Kenya
 Paperback: 9789966258083 \$61/£46/€53

Kamusi Teule ya Kiswahili, Kilele cha Lugha



Kamusi hii ya Kiswahili ni zao la utafiti wa kina uliofanywa na wasomi na waandishi wa kamusi wenye uzoefu. Inalenga wanafunzi wa shule za sekondari, na kwa wasomi wa lugha hiyo, na usomaji wa jumla.

Kurasa 42 za habari ya ziada ni pamoja na:

- Uchanganuzi wa semantik, sintaxical na mofological wa madarasa ya nominoization
- Uainishaji wa maneno k.m. nomino vielezi n.k.
- Istilahi za sarufi ya Kiswahili, Sehemu za hotuba
- Aina za tungo za Kiswahili zinazofundishwa shuleni
- Istilahi zinazotumika katika Fasihi ya Kiswahili -
- Istilahi zinazotumika katika ushairi wa Kiswahili
- Istilahi zinazotumika katika ushairi wa Kiswahili

804 pages | 210 × 148 mm | 2013 | vielelelezovya rangi
 Publisher: East African Educational Publishers, Kenyat
 Paperback: 9789966259363 \$61/£46/ \$61/£46/€53

Vipande vya Dinosaria

Historia ya Msafara wa Kpaleontolojia Kwenda Tendaguru Tanzania

Ina Heumann, Holger Stoecker, Mareike Vennen



Ina Heumann aliongoza mradi wa “Dinosaria huko Berlin”. Anafanya kazi kama mwanahistoria wa sayansi na mweledi wa Historia ya Kipindi Tulichonacho sasa, katika Jumba la Makumbusho ya Historia ya Asili, Berlin. Utafiti wake umejikita katika Siasa ya Historia ya Asili Katika Karne ya Ishirini.

Holger Stoecker ni mwanahistoria na alifanya uchunguzi akiwa Idara ya Masomo ya Kiafrika ya Chuo kikuu cha Humboldt, Berlin, kuhusu historia ya wakati wa ukoloni inayoohusu dinosaria wa Afrika walioko Berlin. Vilevile anashughulika na uchunguzi kuhusu historia ya ukoloni na sayansi kati ya Afrika na Ujerumani na pia utafiti kuhusu asili ya nyara zilizokusanywa kutoka Afrika wakati wa ukoloni.

Kitabu hiki kinasimulia habari za msafara wa kisayansi na nyara zilizopatikana kwenye msafara huo. Masimulizi haya yanaanzia mwanzoni mwa karne ya ishirini, katika kilima cha Tendaguru, kusini mwa nchi ambayo sasa inaitwa Tanzania lakini wakati huo ilikuwa koloni la Wajerumani lililojulikana kama Deutsch-Ostafrika.

Mnamo mwaka 1907, habari za uvumbuzi wa kusisimua wa mifupa, katika kilima cha Tendaguru, ziliufikia Ufalme wa Ujerumani. Muda mfupi baadaye, ikafahamika kwamba kilichovumbuliwa ni visukuku vya mifupa ya dinosaria wakubwa ajabu, wenye ukubwa ambao haujawahi kuonekana, walioishi duniani miaka milioni 150 iliyopita na waliokwisha kutoweka. Miaka michache baadaye, msafara ulioongozwa na wanasayansi wa Kijerumani, ulikwenda mahali hapo na kufanikiwa kuchimbua tani 250 za visukuku vya mifupa hiyo ya wanyama wa zama za kale. Mojawapo ya mapato ya uchimbuaji huo ni kiunzi maarufu kitiwacho Graffatitan brancai ambacho kimewekwa kwenye maonesho ya Jumba la Makumbusho ya Historia ya Asili, Berlin.

Kitabu hiki kinafuatilia hatua kwa hatua mwendo wa visukuku hivyo kutoka kilima cha Tendaguru kwenda pote vilikofikishwa, katika kipindi cha karne ya ishirini. Sura za kitabu hiki, kwa kutegemea vyanzo vya habari kutoka hifadhi za nyaraka za Tanzania, Ujerumani na Uingereza, pamoja na mahojiano, zinauliza, ni kwa jinsi gani historia ya msafara huo imekuwa ikisawiriwa hadi wakati wa sasa. Kitabu kinaonesha jinsi historia ya nyara hizo zilizopatikana Tendaguru inavodhihirisha muingiliano baina ya siasa, sayansi na majumba ya makumbusho, ulivyoyapa sura majadiliano na mabishano; mawasilisho na ufahamu uliopo hadi leo kuhusu Giraffatitan brancai.

236 pages | 303 × 220 mm | 2020 | vielelelezovya rangi

Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania


Hardback: 9789987084869 \$45/£30/€32

Historia ya Kiziba na Wafalme Wake

Tafsiri ya Amakuru Ga Kiziba na Abamkama Bamu

Mfasiri: Galasius B. Kamanzi

Mhariri: Peter R. Schmidt



Historia ya Kiziba na Wafalme Wake: Tafsiri ya Amakuru Ga Kiziba na Abakama Bamu ni mchango mkubwa kwa fasihi ya kihistoria ya wenyeji wa Afrika ya Mashariki na Tanzania.

Utafiti wa Mfalme Mutahangarwa wa Kiziba (aliyetawala 1903–1916) katika mwanzo wa karne ya ishirini ulikusanya mabingwa wa simulizi za mdomo kutoka katika koo za kifalme na zisizo za kifalme na shuhuda zao ziliandikwa na watu waliokwisha kujua kusoma na kuandika, akiwemo F.X. Lwamgira. Miongo mine baadaye matokeo ya utafiti huo yalipigwachapa kikatolea kitabu chenye kurasa 490 katika lugha ya Kihaya ambacho kilibaki bila kujulikana ingawa kilikuwa kitabu muhimu. Tafsiri hii muhimu itafanya historia ya Kaskazini Magharibi mwa Tanzania na Kusini Magharibi mwa Uganda kabla na mwanzoni mwa ukoloni iwafikie kwa mara ya kwanza wasomi wengi.

Mtfsiri **Galasius B. Kamanzi** ni mwanafunzi wa muda mrefu wa historia ya Kiziba na ngano za Kihaya. Yeye ni mwalimu wa zamani na mtumishi wa serikali aliye na B.A. katika Elimu, inayojihusisha na Uchumi na Isimu, kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Alipata pia diploma ya kuhitimu katika Usimamizi Mkuu kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe. Yeye ni mwandishi mwenza wa Folktales kutoka Buhaya.

Peter R. Schmidt ni Profesa Emeritus wa Anthropolojia katika Chuo Kikuu cha Florida na Profesa Maalum wa Anthropolojia na Akiolojia katika Chuo Kikuu cha Pretoria, Afrika Kusini. Yeye ni mwandishi au mhariri wa vitabu kumi na tano juu ya historia ya Kiafrika, mila ya mdomo, urithi, na akiolojia - nyingi zinalenga Buhaya.


476 pages | 229 × 152 mm | 2020

Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania

Paperback: 9789987083695 \$45/£35/€37

Historia ya Jamii ya Zanzibar Na Nyimbo za Siti Binti Saad

Laura Fair



Katika kitabu hicho mwandishi anaelezea jinsi watumwa walivyodai uhuru wao kutoka kwa mabwana zao na jinsi walivyojaribu kudai haki zao kutoka kwa watawala wapya, Waingereza. Baadaye alitafiti visiwa na Tanzania Bara kuhusu historia ya sinema na anatarajia kuchapisha kitabu kingine juu ya sinema hivi karibuni. Kama maprofesa wengi wa zamani katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Fair pia ni mfugaji. Huko Merika anafuga kuku na kondoo bila kutumia dawa (asili) na pamoja na mtoto wake Sabri wanapanda karibu chakula chao chote. Njoo Merika, tembelea vijijini.


120 pages | 210 × 148 mm | 2015

Publisher: Twaweza Communications, Kenya

Paperback: 9789966028396 \$35/£26/€30

Maisha ya Mchagga hapa Duniani na Ahera

Petro Itosi Marealle



Mangi Petro Itosi Marealle, aliyekuwa Mangi Mwitori wa Vunjo, amewafanyia kabila la Wachagga na wazao wa baadaye, kazi ya maana sana kwa kuandika kitabu hiki juu ya desturi za Wachagga kabla hazijatoweka na kupotea. Alijitolea miaka mingi kujifunza kwa uangalifu mila na desturi hizi, na alipata mashaka katika kutafuta njia ya kukichapa kitabu hiki. Ninafurahi kusema amekwisha pata njia. Natumaini kitabu hiki hakitapendwa na Mchagga tu, lakini kila mmoja atakaye kujifunza maendeleo ya Wanadamu, na natumaini kitaamsha WaAfrika wa makabila mengine kutunga habari za namna hii za watu wao. Mwandishi wa kitabu hiki Marehemu Mangi Petro Itosi Marealle alikuwa Mangi wa Marangu kuanzia mwaka 1931 hadi 1946, na 'Mangi Mwitori' wa Vunjo hadi mwaka 1961. Umangi ulipofutwa mwaka 1962 alishika wadhifa mbalimbali katika Halmashauri ya Wachagga na wadhifa wake wa mwisho ulikuwa kama Mwenyekiti wa Tume ya Serikali za Mitaa. Aliafiki mweai Mei, 1982.


132 pages | 230 × 147 mm | 2002

Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania

Paperback: 9789976973914 \$28/£21/€24

Mzee Rukhsa: Safari ya Maisha Yangu

Ali Hassan Mwinyi



Tawasifu hii inafuatia “wasifu wa Mwalimu Julius Nyerere” na “tawasifu ya Rais Benjamin Mkapa” na kuziba pengo lililokuwa limebaki katika kumbukumbu ya awamu tatu za mwanzo za uongozi wa Tanzania huru.

Vitabu hivi vinasaidia kuweka historia sawa; vinaziba baadhi ya mapengo katika kuelewa mambo mbalimbali ya kihistoria. Kitabu kinaitwa “Mzee Rukhsa” kuakisi uongozi wa Rais Mwinyi aliyependa kutumia neno jepesi kama hili kuashiria mambo makubwa aliyokuwa akiyafanya kufungua mipaka ya uchumi na siasa katika Tanzania.

Mojawapo ya mambo yanayowekwa sawa humu, ni kwamba, si kweli kuwa Rais Mwinyi alimkaidi Mwalimu kwa kuanzisha mageuzi kwenye uchumi. Kwa heshima kubwa aliyokuwa nayo kwa Mwalimu, hata akajiona kama ni kichuguu mbele yake aliyemlinganisha na Mlima Kilimanjaro, asingeweza kufanya hivyo. Isitoshe, Rais Mwinyi aliongoza serikali kwa miaka mitano ya mwanzo bila kuvaa kofia ya mwenyekiti wa chama (CCM). Mwalimu asingetaka, yasingewezekana.

Mwalimu alishajaribu kila njia lakini uchumi wa Tanzania uliendelea kudorora. Hazikuwepo fedha za kigeni hata kwa mambo ya msingi kabisa. Mwalimu akampa rukhsa Mwinyi kujaribu maarifa mengine. Baadaye yalikuwapo mambo ambayo Mwalimu hakuyafurahia, akayakemea hadharani. Lakini kimsingi alikubali hoja ya mageuzi, ikiwemo kufungua uchumi kwa sekta binafsi ya ndani na nje ya nchi.

Kadhalika kwenye siasa. Mwalimu aliona umuhimu wa mageuzi kwenye siasa, ikiwemo mabadiliko yaliyoakisiwa kwenye “Maamuzi ya Zanzibar”. Kitabu kinafafanua ilivyotokea, na kwamba wazo la awali lilikuwa la Mwalimu Nyerere, ingawa baadaye kuna mambo hakuyapenda.

Kitabu pia kinazungumzia changamoto nyingi za urais wa Ali Hassan Mwinyi, ikiwemo ile ya muundo wa muungano; migomo; uzawa na chuki baina ya wafanyabiashara; migogoro ya kidini na kadhalika. Yote hayo na mengine yamewekwa vizuri katika lugha nyepesi ya kueleweka na kila mtu.


512 pages | 229 × 152 mm | 2020 | vielelelezovya rangi

Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania

Hardback: 9789987084364 \$55/£40/€42

Peter DM Bwimbo: *Mlinzi Mkuu wa Mwalimu Nyerere*

Peter D.M. Bwimbo



Mtafsiri **Galasius B. Kamanzi** ni mwanafunzi wa muda mrefu wa historia ya Kiziba na ngano za Haya. Yeye ni mwalimu wa zamani na mtumishi wa serikali aliyeye na B.A. katika Elimu, inayojihusisha na Uchumi na Isimu, kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Alipata pia diploma ya kuhitimu katika Usimamizi Mkuu kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe. Yeye ni mwandishi mwenza wa Folktales kutoka Buhaya.

Peter R. Schmidt ni Profesa Emeritus wa Anthropolojia katika Chuo Kikuu cha Florida na Profesa wa Ajabu wa Anthropolojia na Akiolojia katika Chuo Kikuu cha Pretoria, Afrika Kusini. Yeye ni mwandishi au mhariri wa vitabu kumi na tano juu ya historia ya Kiafrika, mila ya mdomo, urithi, na akiolojia - nyingi zinalenga Haya.

Tarehe 20 Januari 1964 maafisa 15 wa Jeshi la Tanganyika (Tanganyika Army) lililorithiwa kutoka serikali ya kikoloni ya Tanganyika, Colito Barracks (Kambi ya Lugalo) waliongoza maasi ya kijeshi dhidi ya serikali ya Tanganyika.

Kikundi kimoja kilikwenda Ikulu kutaka kumlazimisha Rais Nyerere kukubali matakwa yao. Haijulikani ingekuwaje kama kingefanikiwa, na kama Rais Nyerere angeyakataa madai yake. Lolote lingetokea na historia ya Tanzania na ya Afrika ingeathirika vibaya mno. Kwa ujasiri na ubunifu makini, Peter Bwimbo, aliyekuwa mkuu wa kitengo cha ulinzi wa viongozi, (Presidential Security Unit) na mlinzi mkuu (Bodyguard) wa Rais Nyerere, iliwahamisha Rais Nyerere na Makamo wake Rashis Kawawa, akawapeleka mahali salama, akawaepusha hatari, pengine ya kuuawa. Hiyo ndiyo iliyoitwa Operesheni Magogoni. Katika kitabu hiki, Peter Bwimbo, kwa maelezo yake mwenyewe ametoa siri ambayo ni wachache sana waliyoifahamu; haya ndiyo maelezo sahihi ya mbinu alizotumia kuwaokoa viongozi wa nchi.

Kitabu hiki pia ni historia ya Peter Bwimbo, na ya Kitengo cha ulinzi wa viongozi katika Idara ya Usalama wa Taifa. Historia hiyo inaeleza mambo mengi pia kuhusu Tanganyika na Tanzania katika vipindi mbalimbali; jinsi viongozi wa TANU walivyojaribu kuzuia asiwe mlinzi wa Rais kwa sababu alikuwa "jasusi" wa wakoloni katika Special Branch; jinsi Mwalimu alivyoingia kati na kumaliza fitina hiyo; sifa za kazi ya ulinzi wa Rais (ujasiri, umakini na uwezo wa kufanya uamuzi sahihi na haraka, na uzalendo wa kuwa tayari kujitua muhanga ili kumlinda) na mengine. Kutokana na matatizo ya kinidhamu na uadilifu yaliyoikumba Idara ya Usalama wa Taifa, mwaka 1975 Mwalimu aliamua kuwastaafisha viongozi wote wa juu katika Idara ya Usalama wa Taifa, licha ya kuwa alifahamu kuwa Peter Bwimbo hakuwa na dosari yoyote, na hasahasa alikuwa mbele katika kufichua madhambi yaliyokuwa yakitendeka Idarani. Mwaka 1978 alipewa kazi katika Shirika la Reli kuanzisha kitengo cha Usalama, kazi iliyokuwa muhimu sana wakati wa Vita ya Kagera. Mwaka 1985 alipewa Nishani ya Ushupavu (Gallantry Medal) kwa ujasiri wake wakati wa Operation Magogoni na uaminifu wake katika kazi ya Bodyguard wa Rais Nyerere.


476 pages | 229 × 152 mm | 2020

Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania

Paperback: 9789987083695 \$45/£35/€37

Mfinyanzi Aingia Kasri: *Siti Bint Saad, Malkia wa Taarab*

Nasra Mohamed Hilal



Wapenzi wa muziki wa Taarab wana deni kubwa kwa mwinbaji maarufu Siti Binti Saad mzaliwa wa Unguja, ambaye katika uhai wake na baadaye, amejulikana kama Malkia wa Taarab. Malkia huyu aliuchukua muziki wa Taarab akaupa sura mpya, akaubeba na kuufikisha katika ngazi ya kimataifa. Licha ya kuwa waimbaji wengi wa Taarab wamekuja na kuondoka, hakuna ambaye amefikia kilele alichofika Siti Binti Saad. Hayati Shaaban Robert, ambaye nae alikuwa na kipaji cha pekee katika uwanja wa ushairi kwa lugha ya Kiswahili, alihusudu uimbaji na kushangilia maendeleo ya Siti kiasi cha kuandika kitabu juu yake. Kitabut hicho, 'Wasifu wa Siti Binti Saad' ndicho kilichochora, kwa mara ya kwanza picha halisi ya Siti Bint Saad kama ilivyojulikana kwa machache waliomuenzi na waliotaka kuweka kumbukumbu yake kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

91 pages | 207 × 145 mm | 2007


Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania

Paperback: 9789987449460 \$27/£20/€23

Mikidadi wa Mafia

Maisha ya Mwanaharakati na Familia Yake Nchini Tanzania

Pat Caplan



Wazo la kuandika kitabu hiki limetokana na uhusiano wangu na kisiwa cha Mafia Tanzania, ulioanza takriban miaka arobaini na tano iliyopita. Katika muda huo nimetembelea Mafia mara saba na nimeandika na kuchapisha makala na vitabu vingi. Baadhi ya watu wanaoishi kisiwani wamekuwa rafiki zangu wa karibu; mmoja wao ambaye nilimjua vizuri tangu kukutana kwetu mwaka 1965 akiwa kijana mdogo ni Mikidadi Kichange. Tangu kifo chake cha ghafla mwaka 2002 alipokuwa na umri wa miaka arobaini na tisa tu, nimetafakari jinsi anavyoweza kukumbukwa kwa kuandika kitabu kuhusu maisha yake, na kuonyesha mabadiliko makubwa yaliyotokea kisiwani Mafia na nchini Tanzania kwa jumla tangu ipate uhuru. Kitabu hiki ni wasifu wa kihistoria kwa upande mmoja na historia kwa kupitia wasifu kwa upande mwingine, ambamo maisha ya watu wa kawaida yanaonesha mapambano yao na maisha, changamoto, na katika mfano huu uwezo wa ajabu walio nao wa kuyashinda yote yanayowakabili.


190 pages | 229 × 152 mm | 2014

Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania

Paperback: 9789987082957 \$28/£21/€24

Uongozi Wetu na Hatima ya Tanzania

Julius Nyerere



Julius Kambarage Nyerere alikuwa kiongozi wa serikali wa Tanzania ambaye aliwahi kuwa kiongozi wa Tanzania, na hapo awali Tanganyika, kutoka 1960 hadi kustaafu kwake mnamo 1985.

Julius Kambarage Nyerere alikuwa kiongozi wa kwanza wa serikali wa Tanzania na kabla ya hapo wa Tanganyika, kutoka 1960 hadi kustaafu kwake mnamo 1985.

Kitabu hiki kinaelezea matatizo mazito yanayowakabili Watanzania, na kinalenga hasa masuala yanayohusiana na Muungano, uadilifu na utulivu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, kinajadili changamoto za muungano ambazo ni matokeo ya mfululizo wa kupinga uhalali wake chini ya Katiba ya Muungano.

Kitabu hiki kinaelezea sababu za uamuzi wa awali wa kuanzisha muundo wa Serikali Mbili na kusesitiza kwamba, tarehe 26 Aprili 1964, nchi mbili huru ziliachilia haki zao za kuwa Jamhuri na kuunda nchi moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kusaini Mkataba wa umoja huo. Hii ilikuwa kweli kwa Tanganyika, ambayo haikubaki na Serikali yake, ili kuanzia hapo na kuendelea kutokuwa na Serikali yoyote tofauti na ile ya Muungano. Pia, ilikuwa kweli Zanzibar, ambayo ina Serikali tofauti na mamlaka ya kukabiliana na masuala yote yanayohusiana na Zanzibar ambayo hayakuhamishiwa katika Serikali ya Muungano

98 pages | 178 × 127 mm | 2016

Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania

Paperback: 9789987753420 \$24/£18/€21




Uwazi na Ukweli Kitabu cha Kwanza

Rais wa Watu Azungumza na Wananchi

Benjamin W. Mkapa

Hotuba hizo ni ufunguo wa uelewa sahihi wa siasa, uchumi na masuala ya jamii katika nchi yetu katika kipindi hiki cha historia. Umoja wa taifa, mshikamano na juhudi za maendeleo yanahitaji kipaumbele maalum katika dunia ya leo ya utandawazi, na Rais Mkapa anaeleza kwa ufasaha ni nini tunapaswa kufanya ili tuweze kufanikiwa.

138 pages | 205 × 143 mm | 2004 | Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania
Paperback: 9789987417421 \$30/£22/€26




Uwazi na Ukweli Kitabu cha Pili

Rais wa Watu Azungumza na Wananchi

Benjamin W. Mkapa

Rais Mkapa anaeleza kwa kina maana na athari za utandawazi kwetu kama taifa na kwa watu binafsi. Aidha anaendelea kueleza, kufafanua na kutetea sera ya ubinafsishaji na kuonyesha matunda ya sera hiyo bila kupuuzwa sokomoko kama lile lililofuatia hatua ya kubinafsisha shirika la TANESCO.

194 pages | 203 × 127 mm | 2002 | Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania
Paperback: 9789987686766 \$30/£22/€26




Uwazi na Ukweli Kitabu cha Tatu

Rais wa Watu Azungumza na Wananchi

Benjamin W. Mkapa

Kitabu hiki kitawafaa Watanzania wote hasa wanapotaka kufuatilia kwa karibu utendaji kazi wa serikali waliyoiweka madarakani. Ni kumbukumbu muhimu kwa maendeleo ya Taifa na Katika Kuelewa masuala ya siasa, jamii na uchumi wa jamii ya Tanzania.

138 pages | 205 × 143 mm | 2004 | Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania
Paperback: 9789987417421 \$30/£22/€26



Uwazi na Ukweli Kitabu cha Nne

Rais wa Watu Azungumza na Wananchi

Benjamin W. Mkapa

Hiki ni Kitabu cha Tano na cha mwisho katika mfululizo wa vitabu vya Uwazi na Ukweli. Mfululizo huu una malengo makuu matatu: Kwanza ni kufanya mihadhara kuwa moja ya vyanzo vya elimu ya ziada, haswa juu ya maswala anuwai ya kitaifa na kimataifa, sababu na mwelekeo wa maswala hayo.

138 pages | 205 × 143 mm | 2004 | Publisher: Mkuki na Nyota Publishers, Tanzania
Paperback: 9789987417421 \$30/£22/€26



African Books Collective

African Books Collective ni duka la vitabu linalomilikiwa na wachapishaji wa vitabu Waafrika, linalouza na kusambaza ulimwenguni vitabu vya waandishi wasomi, fasihi na vitabu vya watoto.

Lilianzishwa, linamilikiwa na kudhibitiwa na kikundi cha wachapishaji wa Kiafrika wanaozingatia maadili ya tamaduni za Kiafrika, na kusisitiza umuhimu wa sauti za waAfrika kusikika ndani ya Afrika na kimataifa. Linajumuisha wasomi, waandishi wa fasihi, na baadhi ya wachapishaji wa vitabu vya watoto, taasisi za utafiti, waandishi katika vyuo vikuu, wafanya biashara kubwa na ndogo, Asasi Zisizo za Serikali (NGOs), na mashirika ya waandishi.



Sisi ni Nani?

African Books Collective ni duka la vitabu linalomilikiwa na Waafrika, linaloshughulikia masoko na usambazaji ulimwenguni kote wa vitabu kutoka Afrika – vitabu vya kitaaluma, fasihi, na vya watoto. ABC ni ushirika unaomilikiwa na wachapishaji waanzilishi wake. Wachapishaji hao huchagua Baraza la Uendeshaji linalokutana mara moja kwa mwaka. Baraza hilo lina wajibu wa kuweka mikakati ya ABC na uwakilishi wake kwenye uigo mpana wa vitabu na dunia ya uchapishaji. ABC imesajiliwa Uingereza kama kampuni isiyo na lengo la faida na yenye kikomo cha dhamana. Lengo la ABC ni kuwatafutia faida wachapishaji wake na siyo kujitafutia faida.

Historia

Mwaka 1985 kikundi cha wachapishaji walikutana kujadili changamoto zilizokuwa zikiwakabili katika kuuza na kusambaza vitabu vyao nje ya masoko yao ya ndani. Walianzisha ABC kama jitihada ya kuijsaidia wao wenyewe, katika kuimarisha biashara zao na kukidhi mahitaji ya maktaba na wanunuzi wengine wa vitabu. Kwa ufadhili wa mashirika ya kimataifa ya misaada mwanzoni, biashara ilianza mwaka 1989. Mwaka 2007, mabadiliko makubwa katika uendeshaji wake yalifanywa na ikaanza kujitegemea kifedha. Fursa mpya zilijitokeza kutokana na maendeleo ya uchapishaji wa kidijitali na vitabu vya kielektronik, zikachangamkiwa, ABC ikiongoza katika kuweka utajiri wa utamaduni wa kiAfrika katika mfumo wa kidijitali. Pamoja na kwenda na mabadiliko na mbinu yanayojitokeza, sababu na malengo ya kuianzisha bado yako palepale na ABC imeendelea kutolenga kutengeneza faida kwa ajili yake yenyewe.

Personnel

Ofisa Mtendaji Mkuu Justin Cox | justin.cox@africanbookscollective.com

Msaidizi wa Wateja, UK David Brooks | orders@africanbookscollective.com

Msaidizi wa Wateja, USA Carolina Bruno | carolina.bruno@africanbookscollective.com

Council of Management

Kiaire Kamau, **East African Educational Publishers**, Kenya

Tapiwa Muchechemera, **Mkuki na Nyota Publishers**, Tanzania

Ibrahim Oanda, **Codesria**, Senegal

Akoss Ofori-Mensah, **Sub-Saharan Publishers**, Ghana

Francois van Schalwyck, **African Minds Publishers**, South Africa

Kwa maelezo kuhusu jinsi tunavyofanya kazi, na jinsi ya kuagiza vitabu, tafadhali tembelea tovuti yetu: <http://www.africanbookscollective.com/faq>